# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## KIKAO CHA KUMI NA MBILI

**24 APRILI, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### KIKAO CHA KUMI NA MBILI – TAREHE 24 APRILI, 2023

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## III. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**145. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUAKALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, upi Mkakati wa Serikali wa kukuza ujuzi na stadi kwa Vijana.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**146. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kujenga soko la kisasa Ikungi.

**147. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Watu Wenye Ulemavu mitaji katika Jimbo la Mbogwe.

**148. MHESHIMIWA DAVID MWAKIPOSA KIHENZILE (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka magari ya kubeba Wagonjwa katika Vituo vya Afya vya Mtwango na Mgololo.

**149. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kukarabati miundombinu ya Hospitali ya Wilaya ya Arumeru.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**150. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni kero zipi za Muungano zimetatuliwa na zipi zimebaki.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**151. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha Ludewa kwa ajili ya Miradi ya Ufugaji Samaki kwenye Vizimba ndani ya Ziwa Nyasa.

**WIZARA YA MADINI:**

**152. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, lini Wananchi wa Kitongoji cha Nyamichele watalipwa fidia kutokana na madhila waliyoyapata kutoka Mgodi wa Barick.

**WIZARA YA AFYA:**

**153. MHESHIMIWA TOUFIQ SALIM TURKY (MPENDAE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mkakati gani wa kutoa elimu kuhusu Ugonjwa wa Saratani nchini.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**154. MHESHIMIWA CHARLES JOHN MWIJAGE (MULEBA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itapeleka meli ndogo ya abiria Muleba pamoja na kutumia meli ya MV Victoria kujaribu masoko ya nchi za Uganda na Kenya.

**155. MHESHIMIWA DUNSTAN LUKA KITANDULA (MKINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mabokweni - Maramba - Daluni - Bombomtoni - Magoma- Korogwe utaanza.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**156. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, nini mkakati wa kumaliza changamoto za ukosefu wa nyumba za Askari, magari na ufinyu wa Ofisi katika Kituo cha Polisi Mlandizi.

**WIZARA YA KILIMO:**

**157. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani wa kuwawekea mazingira mazuri Wakulima wadogo wa kilimo cha umwagiliaji katika Mto Ruvu.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**158. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni Vijana wangapi wa Tanzania wamepata nafasi za masomo nje ya nchi kwa Mwaka 2015 – 2020 na wangapi wanatoka Zanzibar.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**159. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha mifumo ya utoaji leseni katika Sekta ya Utalii ili kurahisisha upatikanaji wa leseni.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc*** |
| **24 APRILI, 2023** | **KATIBU WA BUNGE** |